

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Simu Na: +255 (026) 2963630
Nukushi: +255 (026) 2963629
Barua Pepe: ps@utumishi.go.tz
Tovuti: <http://www.utumishi.go.tz>



Menejimenti ya Utumishi wa Umma
na Utawala Bora,
Jengo la Taaluma Na. 1,
Chuo cha Masomo ya Biashara na Sheria,
Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),
18 Barabara ya Mkalama,
S.L.P. 670,
40404 DODOMA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

MHE. MWANJELWA AWATAKA WATUMISHI WA TaGLA KUWA WABUNIFU ILI KUWAVUTIA WATANZANIA KUPENDA KUTUMIA MAWASILIANO KWA NJIA YA VIDEO NA KUIPUNGUZIA SERIKALI GHARAMA

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Mary Mwanjelwa (Mb) amewataka watumishi wa Wakala wa Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA) kutumia taaluma yao kubuni mbinu mbalimbali zitakazovutia taasisi za umma, sekta binafsi na watanzania kwa ujumla kupenda kutumia mifumo ya TEHAMA ili kuingezea Serikali mapato na kupunguza gharama.

“Mkiwa kama wataalam wa masuala ya mawasiliano kwa njia ya video na mafunzo kwa njia ya mtandao, jaribuni kusumbua akili zenu kwa kuweka njia madhubuti zitakazowavutia watanzania kupenda wenyewe kutumia mawasiliano kwa njia ya video na mafunzo kwa njia ya mtandao ili kuendana na teknolojia na kupunguza gharama,” Mhe. Dkt. Mwanjelwa amesisitiza.

Akizungumza na watumishi wa Wakala wa Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA) alipofanya ziara ya kikazi katika wakala huo, Mhe. Mwanjelwa amesema ni lazima watumishi wa Wakala huo wafanye kazi zenye matokea chanya ambazo zitapunguza gharama kwa serikali kama ambavyo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Magufuli anasisitiza.

“Ni lazima tujue kiongozi wetu Mkuu wa Nchi anataka nini katika utendaji kazi wetu, tufanye kazi kwa bidii na kuipunguza serikali gharama zisizokuwa za lazima,” Mhe. Dkt. Mwanjelwa ameongeza.

Aidha, amewapongeza watumishi wa wakala huo kwa kazi nzuri wanayoifanya na kuwataka kuangalia namna bora ya kujitangaza ili kufahamika na kupata wateja wengi watakaotumia mawasiliano kwa njia ya video na mafunzo kwa njia ya mtandao ili kuiongezea serikali mapato.

Aidha, ameahidi kutoa ushirikiano kwa watumishi wa wakala huo katika kutekeleza majukumu yake na kuboresha utuoaji huduma kwa umma.

Katika ziara hiyo, Mhe. Mwanjelwa ameshuhudia teknolojia ya mawasiliano kwa njia ya video kwa kuunganishwa na Chuo cha Utumishi wa Umma Nairobi, Kenya na ofisi yake jijini Dodoma.

IMETOLEWA NA;
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
OFISI YA RAIS (UTUMISHI)
TAREHE 29 MACHI, 2019